

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
CHUO CHA UALIMU BUTIMBA**

**MAAGIZO KWA WANACHUO WA MWAKA WA PILI MUHULA WA KWANZA
TAREHE 31/07/2020**

Ada ya Chuo ni 450,000/= kwa mwaka. Ada hii inaweza ulipwa kwa awamu mbili yaani 225,000/= kwa muhula au unaweza kulipa kiasi chote 450,000/= kwa mwaka. Ada ilipwe baada ya kupata namba ya kumbukumbu (Control number) toka kwa mhasibu wa chuo ndugu Makuru Mohamedi Temambele (0786 441 736).

Michango ya Chuo kwa wanachuo wote ilipwe kwenye akaunti ya michango NMB AKAUNTI Na. 31101200023 yenye Jina Butimba Teachers Training College. Michango hiyo ni kama ifuatavyo:

| NA. | MCHANGO | KIASI | MAONI |
|-----|-------------------------------|-------------------|-----------|
| 1 | Serikali ya wanachuo (SEWABU) | 5,000 | Kwa mwaka |
| 2 | Huduma ya kwanza | 10,000 | Kwa mwaka |
| 3 | Usafi na mazingira | 20,000 | Kwa mwaka |
| 4 | Kukodisha godoro | 10,000 | Kwa mwaka |
| 5 | Michezo | 30,000 | Kwa mwaka |
| 6 | Ulinzi | 30,000 | Kwa mwaka |
| 7 | Ukarabati | 25,000 | Kwa mwaka |
| | JUMLA | 130,000.00 | |

Aidha, ada ya Mtihani wa Taifa (NECTA) kwa wanachuo wa mwaka wa pili miaka miwili shilingi 50,000.00 ilipwe kwenye akaunti tajwa hapo juu kabla ya tarehe 30/08/2020.

MUHIMU SANA:

Mwanachuo aje na 'Bank Pay in Slip' au Stakabadhi inayotolewa na Benki husika. Unatakiwa uje na Stakabadhi/Pay in Slip mbili, moja inayoonesha malipo ya ada na nyingine ioneshe malipo ya michango. Ukichanganya malipo hayo hutarudishiwa fedha yako na itakubidi ulipe mara mbili (fanya malipo sahihi kwenye akaunti husika). Vilevile, stakabadhi za malipo zioneshe jina kamili la mwanachuo husika.

Inashauriwa uwe na kadi ya bima ya Afya kwa ajili ya uhakika wa huduma ya matibabu kutoka katika hospitali yoyote na mahali popote utakapokuwa. Ujapo chuoni uje na Bunda (01) la karatasi (DOUBLE A, NOPA, SMART COPY) na iwapo unadaiwa ada, michango au kifaa chochote kwa mwaka wa kwanza hakikisha unakamilisha.

TANBIHI: Wanachuo wote ambo hawajawasilisha vyeti halisi vya kuhitimu kidato cha Nne (Diploma Miaka 3), kidato cha Nne na Sita (Diploma Miaka 2) hata kama hakikutumika kuomba kujiunga na mafunzo ya ualimu, mnatakiwa kuwasilisha vyeti hivyo chuoni kabla ya tarehe 30/08/2020.



Nicholaus A Magige

MKUU WA CHUO

CHUO CHA UALIMU BUTIMBA

S. L. P. 1411 MWANZA

Nakala: Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Chuo